

Jina.....
Shule.....

Nambari yako.....
Sahihi yako.....
Tarehe.....

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA2
Julai/Agosti 2012
Saa 1 $\frac{3}{4}$

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA ZA MBITA – SUBA – 2012
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E.)

102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA 2
Julai/Agosti 2012
Saa 1 $\frac{3}{4}$

MAAGIZO

- (a) Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (b) Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- (c) Jibu maswali yote.
- (d) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA		

*Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahiliku hakikisha kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kufikia miongo michache iliyopita, ujumbe ulisafirishwa kwa njia zilizochukua muda mrefu sana kufika. Kwa mfano, mtu alipotaka kupiga simu katika nchi jirani barani Afrika, ilimbidi kupertia kwa opareta katika nchi za Ulaya ndipo aunganishwe. Kupigia simu kutoka Gambia kwenda Senegal ilibidi kutumia opareta wa kule London na wa Paris, Ufaransa, na wa Senegal.

Leo hii kuna njia nyingi za mawasiliano zilizo bora, za kutegemewa na zinazofikisha ujumbe kwa kasi sana. Ujumbe ambao ungechukua muda mrefu kuufikisha, sasa unapelekwa kwa sekunde moja. Miongoni mwa njia hizi ni mdahilishi, simu tamba na tuama, faksi, satelaiti, mitandao ya wavuti, n.k. Hamna eneo sasa hivi hata liwe mbali vipi lisilofikika na aina hizi za mawasiliano.

Maendeleo haya ya mawasiliano yamechangia pakubwa sana kuufanya ulimwengu kuwa kijiji kimoja. Sasa kuna uhusiano wa karibu sana miongoni mwa mataifa duniani katika nyanja zote za maisha. Hali hii ndiyo inayoitwa utandawazi au utandardihi. Utandawazi umeleta mabadiliko mengi maishani.

Mojawapo ni utoaji na uzalishaji wa mali. Mabadiliko ya mawasiliano yameruhusu mashirika ya kimataifa kusambaza utoaji na uzalishaji wa bidhaa zao katika maeneo mbalimbali duniani. Hali hii imepunguza ghamama za usafirishaji sana. Bidhaa inayoundwa na kiwanda chenye hakimiliki kilichoko kule New York masafa ya mbali, inaweza kuzalishwa na kiwanda kilicho hapa Nairobi. Bila shaka umesikia kuhusu madawa ya kurefusha maisha ya wahasiriwa wa UKIMWI ambayo yanazalishwa na baadhi ya viwanda vya kutengeneza madawa humu nchini. Kiwanda chenye hakimiliki kipo jijini London.

Viwanda ambavyo vilikuwa katika mataifa tajiri kama vile Uingereza, Ufaransa, Marekani, Ujerumanu na Japani sasa vimeweza kutandaza vitandabui vyake kote duniani. Utandazaji huu hufanywa kwa njia kadhaa. Kwanza, viwanda hivi huvinunua viwanda vilivyoko katika mataifa yanayostawi. Vinaweza kuingia katika **ubia** na viwanda vya mataifa wanakotaka kuhamia, Viwanda hivi vya mataifa yanayoendelea hupatana kuwa watasimamia utoaji na uzalishaji wa bidhaa fulani na kukubaliana namna yn kugawa mapato.

Utandawazi katika sekta ya uzalishaji na utoaji bidhaa umeleta manufaa kadhaa katika nchi zinazoendelea, .Mojawapo ya haya ni kupatikana kwa nafasi za kazi. Pili, bidhaa za nchi zinazoendelea ambazo hazingeshindana na zile za mataifa yaliyoendelea sasa zimepata nafasi

ya kushindana. Halikadhalika, wateja wanafasi ya kupata bidhaa watakayo bila kuvunjwa moyo. Iwapo bidhaa anayohitaji mteja hapatikani katika nchi, inaweza kuagizwa moja kwa moja kutoka kwa kiwanda kingine chenyehusiano nacho. Uagizaji hauchukui muda kutokana na hali ya mawasiliano inayoweza kutegemewa na inayofikisha ujumbe bila kupoteza wakati. Fauka ya haya, wateja hupata uwanja mpana wa kuchagua wanachokihitaji.

Utandawazi umehimiza kustawi kwa mazingira ya mashindano katika utoaji na uzalishaji mali viwandani. **Sasa** hivi hamna nehi yeye uwezo wa kufungia bidhaa za nehi nyingine katika nilpaka yake. Kufanya hivi ni kujitia kitanzi kiuchumi. Lazima nchi zifungue masoko yao. Navyo viwanda vya kimataifa huweza kuwania masoko haya. Matokeo yake ni wateja kufaidika kwa kipata uwanja mpana wa bidhaa za kuchagua. Wateja pia hupata bidhaa za hali ya juu na kwa bei isiyo ghali kutokana na mashindano haya. **Mashindano ya kimataifa ni kama ya paka na panya na kiwanda kisichojifunga nira** vizuri, huwa kinajihatarisha. Kinaweza kujipata kimetupwa nje ya soko na kuangamia.

Manufaa rnengine ya utandawazi ni kuwa watu sasa hivi wanaweza kuwasiliana kwa urahisi na wepesi. Kwa kutumia simu, au mdahilishi, mtu anaweza kuwasiliana na mwenzake popote alipo licha ya masafa. Zaidi ya haya, utandawazi umewawezesha watu kutoka asili mbalimbali kuingiliana na **kutangamana**, Utangamano huu umeweza kuleta umoja baina ya watu kwa kutohoa hisia za ubaguzi.

Hata hivyo utandawazi umetokeza kuwa na madhara. Kwanza uchumi wa nchi nyingi umeibukia kutawaliwa na matukio ambayo hayazihu nchi hizo moja kwa moja. Uvamizi wa kijambazi wa Septemba 11, 2000 kule Marekani uliathiri uchumi wa nchi nyingi sana. Matukio ya vita katika Mashariki ya Kati nayo yamechangia kuzorotesha uchumi wa nchi nyingi hasa zile maskini ambazo zinategemea mafuta kutoka huko ilhali vita hivyo haviwahu siko wala ndewe.

Athari kubwa ya utandawazi yaonekana katika sekta ya kijamii. Tamaduni nyingi za jamii katika nchi maskini zinaendelea kuvurugwa na maadili kuporomoka kutokana na ustawi wa kimawasiliano. Vijana wanaiga kutoka mataifa ya kimaghari bila kuchuja. Si ajabu kuwa vijana wetu wanavaa mavazi **yasiyositiri** uchi wao vizuri na yasiyostahiki kwa jina la ustaarabu. Wavulana nao huzidisha kwa **kutoga** masikio na kusuka nywele usiweze kuwatofautisha na dada zao.

Maswali

1. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alm1)
.....
.....
2. Kwa nini hapo awali watu walipitia opareta walipokuwa wakipiga simu? (alm1)
.....
.....
3. Eleza ubora wa mbinu za mawasiliano ya kisasa zikilinganishwa na za zamani (alm2)
.....
.....
4. Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa mawasiliano (alm3)
 - (i) Yamechangia pakubwa sana kufanya ulimwengu kuwa kijiji kimoja?
.....
.....
 - (ii) Viwanda vilivyokuwa katika mataifa tajiri. . . sasa vinaweza kutandaza vitandabui vyake kote duniani
.....
.....
 - (iii) Mtu anaweza kuwasiliana na mwenzake. . . licha ya masafa.
.....
.....
5. Eleza jinsi ambavyo utandawazi katika sekta ya uzalishaji na utoaji umeziathiri nchi zilizostawi. (alm2)
.....
.....
.....
.....
6. Taja mikakati inayotumiwa na mataifa yaliyostawi kutandaza vitandabui vyao (alm2)
.....
.....
7. Fafanua maana ya mafungu haya kama yalivytumika katika kifungu. (alm4)
 - (i) Utandaradhi
.....
.....

(ii) Kutangamana

(iii) Miongo.

(iv) Yasiyositiri

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu.

Magonja hayo yamewahangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha saria nyakati fulani za histori ya binadamu. Magonjwa haya yaliwauwa maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno “UKIMWI” lilitolewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno “UKIMWI” humanisha Ukosefu wa kinga mwilini, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina kama vile ‘umeme’ na pie ‘ugonjwa wa vijana’. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasiweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini. Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethibitishwa kwamba takriban watu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutkana na kuambukiza virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahedumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima yakuishi, badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishi kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la ~~ku~~^zingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ~~ya~~^z ugonjwa hu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba ~~ya~~^zlitokomezwa kupitia juhudhi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

- (a) Kwa kutumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha aya nne za mwanzo (maneno 60 – 70) (alm11)

Nakala Chafu

Nakala Safi

For More Free KCSE past papers visit www.frekcsepastpapers.com

- (b) Eleza mambo yanayoleta matumaini kwa wagonjwa wa UKIMWI kulingana na
aya mbili za mwisho (maneno 20 – 30) (am4)

Nakala Chafu

For More Free KCSE past papers visit www.frekcsepastpapers.com

3. Matumizi ya Lugha

- (a) Ni fonimu gani haifai kuwa miongoni mwa zingine? Toa sababu. (alm2)

Ng', g, t, k

.....
.....

- (b) Fafanua matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika sentensi ifuatayo. (alm2)

Hakukuletea.

.....
.....

- (c) Tunga sentensi ukitumia nomino inayotokana na kitenzi. (alm2)

Abudu

.....
.....

- (d) Kanusha ukitumia ‘O’ rejeshi. (alm2)

Migomba ambayo hupaliliwa vizuri hunawiri sana.

.....
.....

- (e) Andika katika usemi wa taarifa. (alm2)

Je, tutazuru Mombasa lini? Aboi aliwauliza wanafunzi.

.....
.....

- (f) Ainisha vielezi namna katika sentensi ifuatayo. (alm3)

Walikimbia haraka sana wakilia kwikwikwi.

.....
.....

- (g) Andika katika ukubwa wingi. (alm3)

Mwanamume huyu ana ng'mbe mmoja na mbwa.

.....
.....

- (h) Tumia vinyume vyatya maneno yaliyopigwa mistari katika sentensi ifuatayo. (alm2)

.....
.....

- (i) Tumia kihuishi 'katika' kwenye sentensi kuonyesha:

(i) Mahali

.....
.....

(ii) Wakati

.....
.....

- (j) Changanua kwa njia matawi.

Mapambo yaliyonunuliwa na Bakari ni ya Pakistan. (alm4)

.....
.....
.....
.....

- (k) Kando na kuonyesha king'ong'o hafa toa mfano mwengine wa matumizi ya ritifaa. (alm1)

.....
.....

- (l) Andika sentensi hii katika kauli ya kutendeana.

Farida alimlea mtoto wa Farizana naye Farizana akamlea mtoto wa Farida.

.....
.....

(m) Yakinisha. (alm2)

Msiposoma kwa bidii, hamtafanya vizuri katika mtihani.

.....
.....

(n) Tunga sentensi tatu ukitumia neno harka kama;

(i) Nomino

.....
.....

(ii) Kielezi

.....
.....

(iii) Kitenzi

.....
.....

(o) Toa maana mbili zinazodhiihikira katika sentensi hii. (alm2)

Yeye ndiye mwalimu pekee wa Kiswahili.

.....
.....

(p) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia maagizo ya mabanoni. (alm2)

Wanafunzi wote walipita mtihani isipokuwa mmoja. (Anza Hakuna ila....)

.....
.....

(q) Tumia kitenzi ‘vuka’ kutunga sentensi katika hali ya kuamrisha. (alm1)

.....
.....

(r) Andika sentensi katika hali isyodhiihikira. (alm1)

Aliimba akioga.

.....
.....

(s) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo. (alm2)

(i) Sabuni

.....
.....

(ii) Zabuni

.....
.....

ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Mhusika X: Hebu sema majina ~~gaya~~ yako kamili?

Y: Mussa bin Ma~~ru~~^{ra}suudi.

X: Ulisema ~~anata~~ kukata rufani?

Y: Ikiwezekana.

X: ~~Usitie shaka umepata presidential amnesty.~~

~~Y: Alhamdulillah. Nitaenda Mskitini Ijuma kuabudi na kumshukuru Mungu.~~

Maswali

- (a) ~~(i)~~ Taja muktadha wa mazungumzo haya (alm2)

¹ See, e.g., *United States v. Ladd*, 10 F.3d 1250, 1254 (11th Cir. 1993) (“[A]nyone who has ever been to a bar or restaurant knows that it is common for people to leave a tip for waitstaff.”); *United States v. Gandy*, 10 F.3d 1250, 1254 (11th Cir. 1993) (“[A]nyone who has ever been to a bar or restaurant knows that it is common for people to leave a tip for waitstaff.”).

Digitized by srujanika@gmail.com

(ii) *Toa sababu ya kuthibitisha jibu la (a) hapo juu.*

- (b) Tambua wahuiska X:.....

- (c) Taja na kutoa mifano ya sifa zozote tatu za lugha inayotumika katika

mazungumzo haya. (alm6)

Digitized by srujanika@gmail.com

¹ See, e.g., *United States v. Ladd*, 10 F.3d 1250, 1254 (11th Cir. 1993) (“[A]nyone who has ever been to a bar or restaurant knows that it is common for people to leave a tip for waitstaff.”); *United States v. Gandy*, 10 F.3d 1250, 1254 (11th Cir. 1993) (“[A]nyone who has ever been to a bar or restaurant knows that it is common for people to leave a tip for waitstaff.”).

Digitized by srujanika@gmail.com

Digitized by srujanika@gmail.com

.....

Digitized by srujanika@gmail.com

[View Details](#) | [Edit](#) | [Delete](#)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com